


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU WA MALIPO KWA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inauarifu umma wa Watanzania, Taasisi za Elimu ya Juu, na Wadau wote wa Elimu ya Juu kwamba malipo kwa ajili huduma zinazotolewa na TCU yanafanyika kwa njia ya Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG). Aidha, umma unafahamishwa kwamba, huduma mbalimbali zinazotolewa na TCU zinazohitaji malipo zimeainishwa kwenye tovuti www.tcu.go.tz.

Mwombaji wa huduma atapewa Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (Control Number), na baada ya malipo kufanyika risiti halali ya malipo itatolewa na TCU kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu za malipo ya Serikali.

Ili kurahisisha utoaji wa huduma, TCU imeweka utaratibu rafiki na rahisi kwa mwombaji wa huduma inayohitaji malipo. Mwombaji anaweza kupata Namba ya Kumbukumbu ya Malipo kupitia tovuti ya Tume www.tcu.go.tz au kwa kuwasiliana nasi kwa njia ya simu kwa namba **+255 (0) 22 2113694**.

Hivyo wananchi na wadau wote wanahimizwa kutofanya malipo yoyote nje ya utaratibu huu ili kuepuka matapeli.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
11/08/2020